



TUME LA AFYA YA UZAZI ULIOUNDWA KURATIBU HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI NCHINI KENYA: Kukadiri Huduma Za Kimsingi Zilizopatikana

Hii ni ripoti inayotumiwa na wale wote waliotoa mchango wao, wake, waume na vijana wakati uchunguzi huu ulikuwa ukiendelea. Inakusudia kuwaarifu wahusika wote hao jinsi Tume ya Wanawake (Women's Commission) inatumia habari zilizopatikana katika uombezi na utetezi wa haki za wale walioathiriwa na ghasia za kisiasa zilizozuka baada ya uchaguzi mkuu mapema mwaka huu nchini Kenya.

SISI NI NANI?

Tume ya Wanawake inayoshughulikia Wakimbizi wa Kike na Watoto (The Women's Commission for Refugee Women and Children) ni shirika lisilo la serikali (NGO) ambalo makao makuu yake ni United States, Amerika. Ni shirika la utetezi na uombezi. Hushirikiana na serikali, Umoja wa Mataifa (UN) na mashirika ya kimataifa yanayotoa misaada ili kuhakikisha kuwa haki, usalama na matakwa ya wakimbizi yametiliwa maanani wakati miradi inapoanzishwa na misaada kutolewa. Hatuhusiki katika utekelezaji wa huduma wala hatutoi misaada ya moja kwa moja kwa miradi inayowasaidia wanawake, watoto na vijana. Badala yake, sisi huchangia katika kuwezesha suluhisho la kudumua matatizo yanayowakabili wakimbizi.

KWA NINI TULIFANYA ZIARA KENYA?

Tulizuru Kenya ili kujionea na kujihakikishia kwamba huduma za afya zinazohusu magonjwa ya zinaa, upangaji uzazi na uzima wa jamii zilikuwa zikitolewa kwa wakimbizi wa kike, kiume, vijana na watoto baada ya ghasia za kisiasa zilizotokea baada ya uchaguzi mkuu mnamo mapema mwaka huu. Kuna huduma za afya za kimsingi zinazofaa kutolewa wakati wa jambo la dharura. Tungependa pia kujumuika pamoja na wale waliokuwa wakihudumu pamoja na wakimbizi waliopokea huduma zenyewe. Tulitaka kujionea kilichotendwa na kisichotendwa, vilivyokuwemo na vilivyokosekana. Pia tulitaka kufanya uchunguzi na kujua kuwa wahasiriwa walihitaji vifaa gani ili kuboresha maisha yao.

TULIFANYA NINI TULIPOKUWA ZIARANI?

Wenzetu wawili kutoka Women's Commission (Tume ya Wanawake) walizuru Kenya na wakakaa huko kwa muda wa majuma mawili katika mwezi wa nne (Aprili) mwaka 2008. Tulitembelea kambi mbalimbali za wakimbizi na mahospitali katika Nairobi, Kisumu, Kitale, Eldoret na Nakuru. Tulikutana na watu 139, wake, waume na vijana katika makongamano manane ya wakimbizi kwa majadiliano. Tuliwafanyia hojaji maajenti wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) ya humu nchini na ya kimataifa pamoja na maajenti wa Umoja wa Mataifa (UN), Shirika la Msalaba Mwekundu (Red Cross) na Wizara ya Afya.

Kujumuika katika kikao pamoja na Wakenya kulitupatia nafasi nzuri ya kugundua moja kwa moja kutoka kwa wahasiriwa matatizo na maafa yaliyowakabili wakati wa ghasia za kisiasa baada ya uchaguzi mkuu. Tunashukuru si haba kwa kuweza kujumuika na kwa kuidhinishwa tutumie kwa uajibikaji habari adhimu walizotupatia.

JE, TULIFANYA YEPI TULIPOKUWA KATIKA ZIARA?

Idadi kubwa ya wanawake, wanaume na vijana waliotimuliwa kutoka makwao walijipata katika majaribu magumu. Waliishi katika hali na mazingira yasiyopendeza, hofu ya kurejea makwao, msimu wa mvua nyingi na sintofahamu ya siku za usoni. Katika kambi za wakimbizi nchini mwao, kulizuka magonjwa kama pneumonia, kuharisha na malaria. La kutia hofu zaidi lilikuwa ni madhara yaliyowapata watoto wa shule hasa wale waliokuwa katika shule za upili au sekondari na vyuo. Vijana hao wenyewe walikuwa wakiwanasahi maajenti wawape nafasi na fursa za elimu na kazi. Jambo hili halingewezekana kwani tayari maajenti wengi walikuwa wameanza kujiondokea Kenya masuala haya yalipoanza kukadiriwa.



Tulijaribu kukabiliana na masuala matano adhimu yaliyohusiana na huduma za afya zilizotolewa kwa wahasiriwa:

1. Kama maafisa wawakilishi walikadiriya huduma za afya zilizotolewa kwa wahasiriwa ili kuona kwamba kwa hakika zilipokewa?
2. Hasa ni mipango adhimu gani ilifanywa ili kuzuia na kuhakikisha kwamba dhuluma na hujma za kimapenzi kama ubakaji na kadhalika hazikutokea na zilipotokea waathiriwa walipata huduma gani?
3. Walifanya nini ili kuhakikisa kwamba virusi vya UKIMWI havikuambukizwa au kuenezwa kwa kasi na kiasi kikubwa?
4. Ni mambo gani yaliyofanywa ili kuhakikisha kuwa idadi ya vifo vya kiholela ilipunguka na wajawazito na watoto waliozaliwa katika hali hii walishughulikiwa?
5. Ni mipango kabambe gani iliyokusudiwa ili kuboresha huduma za afya zinazohusiana na magonjwa ya zinaa, upangaji uzazi na uzima wa afya licha ya mengine yanayozuka katika ghasia za kivita na msukosuko?

MATOKEO MAALUM



“Watoto wangu wanatakikana kujiunga na shule ya upili. Marehemu mume wangu alikuwa dereva hapo kabla kuuawa kwake. Sasa sina namna yoyote ya kukidhi mahitaji yangu.”

Haya yalisemwa na mama mmoja aliyeshiriki katika majadiliano katika kongamano la wakimbizi wa kike mjini Kisumu.

Suala nyeti lingine kuhusu vijana lilikuwa ni ongezeko la kitendo cha kujamiiana, kama vijana wenyewe walivyokiri. Baadhi ya vijana walioshiriki katika kongamano za wakimbizi walitoa taarifa kwamba wasichana na wavulana walikuwa wakipatana na kufanya mapenzi aghalabu mara nyingi katika kambi, kinyume na kabla ya ghasia ambapo walipatana tu katika kanisa, hafla mbalimbali na katika sherehe za harusi. Ulazaji damu na uhaba wa nafasi katika hema na kambi zilichangia pakubwa katika jambo hili. Uhusiano huu wa kimapenzi miongoni mwa vijana lilikuwa swala nyeti kwani ulichongea na kuhujumu mila na tamaduni za kiasili.

1. JE, HUDUMA ZA MATIBABU ZILITOLEWA KILA WAKATI?

Wakati maafisa wa mashirika ya kimataifa na ya nchini Kenya walikuwa mikutanoni katika jiji la Nairobi, hakuna lolote lililofanywa kuhakikisha kwamba hujma za kimapenzi ziliendelea kuzuiliwa au hata huduma za afya ziliendelea kutolewa katika kambi. Ukosefu huu ulisababisha mambo mengi kama itakavyofahamika hivi punde.

2. JE, NI NINI KILIFANYWA ILI KUZUIA DHULUMA ZA KIMAPENZI NA KUWASHUGHULIKIA WALIOHUJUMIWA KATIKA JINSI HII?

Dhuluma na hujma za kimapenzi pamoja na kufanya mapenzi ovyo yaliibuka kuwa masuala nyeti miongoni mwa wakimbizi wanawake na wasichana. Baadhi ya maafisa walitoa misaada yao iwapo tu waliruhusiwa kufanya ngono na wahasiriwa hata ingawa wengine wao walikuwa ni wasichana wadogo sana. Hongo pia zilikuwa zikitolewa na kupokelewa sana. Walioshiriki katika kongamano za wakimbizi walituarifu kwamba idadi kubwa ya wanawake na wasichana hawakulala na wanaume kwa sababu ya kuni, maji au chakula bali ili wapate vitu muhimu kwa matumizi ya kibinafsi kama vile chupi, sabuni, mafuta ya kujipaka na manukato. Miongoni mwa maafisa walioendelea vitendo hivi ni polisi, wafanyabiashara, wasimamizi wa kambi na wahudumu kutoka mashirika ya misaada.

Dhuluma zinazofanyiwa jinsia ya kike hujitokeza katika ncha tofauti tofauti. Jambo la dharura na muhimu ni kuhakikisha kwamba zimezuiliwa kabla hazijatekelezwa la sivyo huzidi wakati wa ghasia. Maajenti wengi walikuwa wakifanya kazi chini ya uongozi wa shirika la UN Population Fund (UNFPA) na Shirika la Msalaba Mwekundu (Red Cross) Kenya. Ilitakikana wahakikishe kwamba huduma za kimsingi zilizopendekezwa kimataifa zimetolewa kwa wote waliohasirika kutokana na kuhujumiwa kimapenzi. Maajenti wa Umoja wa Mataifa (UN) waliwapa mafunzo wahudumu wa mashirika ya kitaifa na kimataifa na kwa wale wote walitoka katika taasisi na wizara mbalimbali za serikali. Masuala yaliyohusiana na usalama yalikuwa kama vile ukosefu wa washika doria katika kambi, vyoo visivyofungika kutoka ndani na ukosefu wa taa za umeme.

Katika kambi ya Noigam, mjini Kitale, familia zilipewa kurunzi (tochi). Hata hivyo si familia za wakimbizi wote zilizobahatika kujipatia tochi. Katika Uwanja wa Maonyesho wa Nakuru, taa za umeme hazikuwekwa ingawa zilikuwa zimelipiwa.

Hakuna mikakati yoyote iliyowekwa ili kuzuia mbembe kuajiriwa na mashirika mengine tofauti au hata kurejea kambini licha ya vitendo vyao vya usherati, ingawa maajenti walikuwa wamepewa mwongozo jinsi ya kukabiliana na madhara yanayotokea baada ya kudhulumiwa kimapenzi na namna ya kuripoti dhuluma zenyewe.

Adhulumiwaye kimapenzi huhitaji matibabu na huduma za dharura za afya na uzima ili kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VU) na utungaji wa mimba isiyotakikana. Kuna dawa inayoweza kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VU) endapo itatumiwa kabla masaa 72 kumalizika baada ya kuhasiriwa. Licha ya dawa hii, emergency contraception (uzuiaji mimba wa dharura) ni dawa ambayo ikitumiwa kabla masaa 120 kupita baada ya kitendo cha ngono yaweza kuzuilia mimba kutungika. Dawa hii haiwezi kumdhuru mtu ambaye tayari ni mjamzito. Pia kuna madawa mengine ya kuingia na kutibu magonjwa ya zinaa. Dawa nyingi walizohitaji wakimbizi baada ya tendo la ngono zilipatikana kwa wingi. Ni tu kwamba waathiriwa wengi wa ngono hawakujitokeza kwa kuchelea fedheha na aibu. Pengine hawakuelewa ilivyobidi umuhimu wa kupata huduma za afya kwao. Kuna wengi waliojitokeza polepole miezi sita baada ya kuhasirika. Kwa upande mwingine, nasaha, uelekezaji na ushauri ulitolewa kwa wahasiriwa ingawa ubora wa huduma hizi ulitofautiana kutoka shirika hadi shirika na kutoka mtoaji huduma hadi mwingine.

3. KULIKUWA NA MIKAKATI YA KUPUNGUZIA MAAMBUKIZI YA HIV?

Mengi yangalifanyika ili kuzuia usambazaji wa virusi vya HIV, lakini ilibidi kuteua matendo yaliyofaa zaidi na kuyapa kipaumbele. Moja katika haya bora ilikuwa kugawa mipira ya kondomu iliyotolewa bure. Serikali, wahudumu na wakimbizi wote walielewa kwamba HIV ni ndwele kamili. Mipira ya kondomu kwa wanaume ilipeanwa katika kambi. Pipa za kurusha taka baada ya matumizi pia zilipatianwa. Kuna wale ambao hawakupata mipira ya kondomu japokuwa walikuwa kambini na mipira yenyewe haikuwa adimu.

Kusema kweli madhara ya ghasia za kisiasa zilizotokea baada ya uchaguzi kuhusu ongezeko la maambukizi ya HIV hayajaweza kukadirika barabara.

Serikali ya Kenya pamoja na taasisi za kitaifa na kimataifa walihakikisha kwamba watu waliohitaji dawa za antiretroviral walizitumia ilivyofaa wasije wakapata usugu. Timu iliyokuwa ikikadiriya ilijifunza kutoka mashirika kama Academic Model for the Prevention and Treatment of HIV (AMPATH) kuwafikia wakimbizi kupitia kwa mawasiliano ya simu za siri na simu tamba.



Kifaa cha kurusha taka za kondomu katika kambi ya wakimbizi nchinimwao katika Uwanja wa Maonyesho wa Eldoret.

4. VIFU NA KUDHOOFIKA KWA WAJAWAZITO NA VITOTO VILIVYOZALIWA VILIPUNGUZWA?

Kulipotokea jambo la dharura kama vile kushikwa na uchungu wa kuzaa kwa ghafla, wawakilishi wa mashirika kama vile UNFPA walipeana zana za uzalishaji kwa wajawazito kupitia wenzao kambini. Vifaa hivi viliwezesha mazingira safi ya kuzalia badala ya nje, ndani ya magari ya usafiri, katika mahema n.k. Pia vifaa hivi vilitolewa kwa vituo vya afya vya karibu endapo hawakuwa navyo. Miongoni mwa vifaa hivi ilikuwa ni chandalua, glavu, sabuni, wembe, kamba ndogo au uzi wa kufunga kitovu, mfuko wa kurusha taka, picha ya kielelezo na nguo. Mashirika ya kimataifa na ya kitaifa ndio waliogawa vifaa hivi katika kambi mbalimbali ingawa vifaa vyenye haviikutosha. Wanawake wote tuliofanyia hojaji katika kongamano zetu hawakuwa wamevitia machoni vifaa kama hivi, wala kusikia kuwepo kwake.

Jambo jingine liliosaidia katika upunguzaji wa vifo na kudhoofika ilikuwa ni kuwashughulikia wajawazito waliokuwa na mimba zenye usumbufu na waliohitaji msaada katika kliniki zilizosheheni vifaa vya uzalishaji. Ili kuwezesha jambo hili, ilibidi watu miongoni mwa jamii wajue na waweze kuzitambua dalili katika mjamzito zilizoashiria hatari na zilizohitaji huduma za dharura. Ni sharti kungekuwepo na namna ya kumsafirisha mjamzito pindi tu ilipotambulikana kuwa alihitaji kusaidiwa. Lazima kituo cha afya alichopelekwa kingekuwa na vifaa adhimu vya uzalishaji na wahudumu wenye ujuzi wa ukunga. Tume ya wanawake (Women's Commission) ilitanabahi kuwa suala la usafiri lilikuwa nyeti hasa katika kambi iliyokuwa mjini Kitale kulikokuwa kumetangazwa hali ya kutotoka nje. Iliwabidi maafisa kuomba kibali cha usafiri kutoka shirika la Msalaba Mwekundu (Red Cross). Matatizo mengine yalikuwa ukosefu wa magari, petroli, madereva na milango iliyofungwa nyakati za usiku. Ilifahamika kwamba katika kambi moja mjini kitale maafisa wa Red Cross walikuwapo mchana tu na iwapo hali ya dharura ingetokea usiku, hakuna msaada wa kiasi cha haja ungeweza kupatikana, isipokuwa kusubiri hadi asubuhi.

"Kulikuwa hakuna magari ya kusaafiria na kwa hivyo iliwabidi majirani watayarisha baisikeli.

Alivuja damu sana na baada ya kuwasili hospitalini, hakushughulikiwa sana.

Hatimaye saa kumi na mbili alfajiri mama huyo na kitoto chake waliaga dunia. Marehemu alikuwa na umri wa miaka 38."

Taarifa hii iliripotiwa na mshiriki mmoja mwanamume katika kambi mjini Kisumu.

Serikali ya Kenya pamoja na taasisi za kitaifa na kimataifa walihakikisha kwamba watu waliohitaji dawa za antiretroviral walizitumia ilivyofaa wasije wakapata usugu. Timu iliyokuwa ikikadiriya ilijifunza kutoka mashirika kama Academic Model for the Prevention and Treatment of HIV (AMPATH) kuwafikia wakimbizi kupitia kwa mawasiliano ya simu za siri na simu tamba.

5. JE, NI MIKAKATI GANI ILIYOKUWEPO ILI KUWEZESHA HUDUMA MBALIMBALI ZILIZOHITAJIKA LICHA YA ZILE ZA AFYA?

Masuala mengine yaliyogusiwa ni upangaji wa uzazi na kujidhibiti wakati wa hedhi. Katika majuma ya mwanzo mwanzo, maajenti waliripoti kuadimika kwa madawa na vifaa vingine vya upagaji wa uzazi kutokana na ukosefu wa usalama nchini. Wakati utafiti huu ulipokuwa ukifanywa kliniki za serekali na za mashirika yasiyo ya kiserekali (NGO) zilikuwa zimeanzisha huduma za upangaji wa uzazi. Marie Stopes



Gari la ambulanzi hapo nje mwa kliniki katika kambi ya wakimbizi nchini mwao katika Uwanja wa Maonyesho wa Eldoret.

JE, SASA TUME YA WANAWAKE (WOMEN'S COMMISSION) ITAFANYA NINI?



ya Kenya walikuwa wakisambaza huduma zao kupitia kwa maajenti wao walioshirikiana na maajenti wengine waliokuwa kambini ili kutoa huduma za upangaji wa uzazi za kudumu kama vile kufungwa kabisa kwa wanaume (vasectomy) na kufungwa kabisa kwa wanawake (tubal ligation). Walioshiriki katika kongamano zetu za wakimbizi walionelea kuwa lilikuwa ni jambo bora kabisa kuwapo na upangaji wa uzazi kambini kwa sababu ya hujuma za kimapenzi zilozofanyiwa baadhi ya wakimbizi nchini mwao. Pia, ilitokea kwamba ongezeko la mimba lilizidi baada ya ghasia za kisiasa. Upangaji uzazi ni jambo ambalo halikuwa na budi na lilibidi. Katika Uwanja wa Maonyesho wa Nakuru, uavyaji wa mimba haramu uliripotiwa.

"Huduma za upangaji uzazi zinazidi kuhitajika kwa kuwa watu hawajui kitakachowafanyikia siku za mbeleni."

Kongamano la wakimbizi wa kike katika kambi ya Noigam, mjini Kitale.

JE, SASA TUME YA WANAWAKE (WOMEN'S COMMISSION) ITAFANYA NINI?

Tume ya wanawake inayoshughulikia maswala ya wakimbizi wa kike na watoto itajadili matokeo ya utafiti huu na kisha itatoa mapendekezo yao kwa serekali, wafadhili, Umoja wa Mataifa (UN) pamoja na kwa mashirika ya kimataifa na maajenti wa kitaifa. Baadhi ya mapendekezo yatakuwa uombezi na utetezi wa:

- Kuwapo na kliniki zitakazoshughulikia afya na upangaji wa uzazi na magonjwa ya zinaa katika UNFPA na katika Wizara ya Afya, ambazo zingali zahitajika kwa sababu watu wanaendelea kuwa wakimbizi katika kambi na miongoni mwa jamii, wengine wakisubiri kurudi kwao au wakiwa katika hali ya taharuki baada ya kurejea kwao.
- Maajenti wote wafaa wajihami kikamilifu ili waweze kuzuia hujuma na dhuluma za kimapenzi na waweze kuhudumu barabara na kudumisha nidhamu; wajulishe jamii wanayoihudumia ni wapi na ni vipi wanaweza kuripoti visa vya hujuma za kimapenzi na umuhimu wa kupata matibabu mtu anapodhulumiwa kimapenzi..
- Maajenti wote wa wizara ya afya, au wafadhili wa sekta ya Afya wafaa kutilia rutuba mipango kabambe ya huduma za afya ili kuweza kukabiliana na mimba na kutoa huduma bora kwa wale wanaokuwa na mimba zenye matatizo. Haya ni adhimu hasa sasa ambapo mashirika yanaipatia serekali na mashirika ya kitaifa miswada yao.
- Mashirika yote yahakikishekuwa vijana wameshughulikiwa kikamilifu katika kurudishwa katika nadhari na hali ya kawaida na pia kuboresha fursa na nafasi zao katika elimu na kazi.

JE, UTAFANYAJE IKIWA UNGEPENDA KUJUA ZAIDI KUHUSU SHIRIKA LETU NA KAZI TUFANYAYO?

Kwa kupata nakala ya ripoti kamili, tafadhali wasiliana na; http://www.womenscommission.org/pdf/ken_misp.pdf

Endapo ungependa kujua zaidi kuhusu Tume ya Wanawake inayoshughulikia wakimbizi wa kike na watoto na vijana, wasiliana na mtandao wetu www.womenscommission.org au uwasiliane nasi katika

Ripoti hili lilitafitishwa na kuandikiwa na Mihoko Tanabe, mbunifu wa miradi ya afya ya uzazi, na Sandra Krause, mkurugenzi wa miradi ya afya ya uzazi, Tume ya Wanawake inayoshughulikia Wakimbizi wa Kike na Watoto. Ripoti hili limetafsiriwa na Bi Josephine Kirubi, na kusomwa na Juliana Bol.

Tume la Wanawake linashukuru Jedidah Mwawingwa, aliyetafsiri makongomano. Mradi huu haugewezekana bila ushiriki wa wakimbizi wa kike, kiume na vijana wa Kenya, waliotupa maarifa, visa, fursa na vidokezo maalum.

Ukadiri huu uliwezekana kwa msaada karimu wa Wakfu wa William na Flora Hewlett.

Picha zote:Tume ya Wanawake inayoshughulikia Wakimbizi wa Kike na Watoto /Sandra Krause



Women's Commission for
Refugee Women and Children
122 East 42nd Street
New York, NY 10168-1289
212.551.3115
info@womenscommission.org

Septemba 2008